



Yaliotokea Kuzunguka Kifo Cha Yesu
Na Tam Raynor

Yaliyomo

Masomo:	Uka.
1. Kusudi La Msalaba	3
2. Usaliti	5
3. Kusiko	7
4. Kukana	9
5. Chaguo	12
6. Kuuliza	14
7. Kusulibishwa	16
8. Kifo	20
9. Mwana Kondoo Aliyekimya	22
10. Ufufuo	24
11. Kanisa Mwili Wa Yesu	26
12. Marejeo Ya Pili	28

Kusudi la Msalaba

1. Msalaba ulikuwa katika nia ya Mungu tangu mwanzo. Efe. 3:10-11
 - A. Kwa nini?
 - a. Wanadamu walipewa uhuru wa kutii au kutomtii Mungu
 - b. Kwa sababu tunge asio Mungu alikuwa na mpango katika nia yake wa kutosamehe
 - B. Kutotii kungesababisha kifo. Mwa. 2:17
 - a. Wote tuna nafasi ya kutii au kutotii.
 - b. Mara nyingi kila mmoja wetu anachagua kutotii. Rum. 3:23
 - c. Mungu alisema kwamba kutotii matokeo yake yatakuwa kifo. Rum. 6:23
2. Njia pekee ya kuepuka kifo ni lazima kitu fulani au mtu fulani afe, kwa niaba yetu.
 - A. Mungu alimfundisha Adamu na Hawa namna ya kuua wanyama wao walio bora, kuwateketeza juu ya madhabahu ili awezekuwasamehe maovu yao.
 - B. Kaini na Habili walikuwa wanafanya hivyo. Tunajifunza kwamba mazao hayaleti msamaha bali ni damu tu. Mwa. 4:3-5
 - C. Mungu aliwafundisha waisraeli, jinsi ya kuua wanyama wao walio bora, na kuinyunyizadamu kuizunguka madhabahu, na kuiteketeza mwili wake. Law. 1
 - a. Wanyama walio bora, nao ni mafahari (ng'ombe dume asiye hasiwa), kondoo, mbuzi tu.
 - b. Damu nyingi sana.
 - c. Miili mingi ya kuteketezwa.
 - i. Je, hili halionekani kama upuuzi? Maangamizi ya vilivyo bora, maangamizi ya vile vinavyopaswa kuokolewa na mbinguni?
3. Tatizo: Damu ya wanyama haitoshi kusamehe dhambi za mwanadamu. Ebr. 10:4
 - A. Kwa nini? Kwa sababu wanyama siyo watenda dhambi. Wanyama hawana hatia ya dhambi
 - B. Mwanadamu ndiye mwenye dhambi, ndiye anayepaswa kufa kwa sababu ya kile alichokifanya
 - C. Mwanadamu ndiye anayestahili kifo
4. Mpango:
 - A. Tangu mwanzo mpango wa jinsi gani mwanadamu ambavyo angeokolewa ulipangwa
 - a. Kuna Unabii 369 juu ya dhabihu hii kuu! Mifano:
 - b. Zaburi 2:1, 6-8, 12-18—Kuchomwa kwa mikono na miguu, watu wengi walihusika, kifo cha kufa pole pole
 - c. Isaya 53:3-12—Angepigwa, damu yake ingemwagwa, kaburi lake lingekuwa pamoja na kaburi la matajiri, angeuawa na waovu, asingepigana kwa ajili ya uhai wake, angekuwa kama mwanakondoo, asiye na hatia ya dhambi
 - d. Zaburi 41:9—Atasalitiwa na rafiki
 - e. Zekaria 11:13—Vipande thelathini vya fedha vingepigwa hali hii ya kusaliti, kisha vingepigwa shamba la mfyanzi
 - B. Unabii unaendelea na kuendelea juu ya mtu huyu mkuu namna atakavyokufa na kuwaokoa wanadamu kutoka kwenye maangamizi
5. Mtu huyu mkuu angekuwa Mungu Mkuu Mwenyewe Isaya 9:6
 - A. Mungu Mwenyewe alikuwa tayari kujitoka dhabihu mwenyewe ilikutuokoa kutoka kwenye kifo alichotuahidi
 - a. Alimtuma mtoto wake azaliwe kama mwanadamu, chini ya sheria ya dhambi na mauti, ili afe, amwage damu yake, ilituweekwe huru toka kifoni
 - b. Yesu alisema alikuwa Mungu, Yohana 8:58 (“Mimi Ndiye” ni jina la Mungu)
 - B. Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, na Yesu alitabiri juu ya dhabihu yake
 - a. Mathayo 26:26-25—Yesu alimjua atakaye msaliti
 - b. Mathayo 26:26-29—Yesu alijua kwamba damu yake ingemwagwa, na ingeanzisha sheria mpya, mkataba mpya
 - c. Mathayo 12:40—Yesu alijua kwamba atauawa, atazikwa, na kufufuliwa katika siku ya tatu.
 - C. Sababu nzima ya Yesu kuwa duniani ilikuwa ni kutimiza mpango wa Mungu wa kunmwokoa mwanadamu kutoka kwenye maangamizi

- a. Njia pekee ya kumwokoza mwanadamu ilikuwa ni kwa kumwaga damu Ebr. 9:22
- b. Mfano: Waisraeli wakiwa Misri. Usiku wao wa mwisho, walitakiwa kunuua mwanakondoo, na kupaka damu yake kwenye miimo ya mlango ya nyumba zao, ilikwamba malaika wa mauaji apite juu ya nyumba zao na asiue mzaliwa wao wa kwanza.
- c. Tunapaswa tujioshe, na damu ya Yesu ipakwe kwenye miimo ya mlango wa mioyo yetu, ili kwamba malaika wa mauaji apite juu yetu pia. Yesu ndiye mwanakondoo wetu leo.
Kwa nini? 1 Kor. 5:7

6. Kwa sababu Mungu anatupenda sana. Yohana 3:16

- A. Tunampenda kiasi gani? Je, tunampenda vyakutosha hata tumtii? Au tunampenda kwa kutomtii?

Usaliti

Math. 26:14-16; 20-25; 47-50; Math 27:3-10

Mpango ulikuwa kwamba Yesu afe kwa ajili ya dhambi zetu. Yesu angeonekana hana akili kama angetembea mbele ya Pilato na kusema, “Nisulibishe ili niwasamehe watu dhambi zao!” Pilato angefikiri kwamba Yesu alikuwa na matatizo ya akili! Hamna mtu ambaye angeelewa kwamba Yesu anakufa kwa ajili ya dhambi zao. Watu wengine wamekuwa wanakufa misalabani kwa miaka mingi na wote walikuwa wa harifu. Hawakumsulibisha mtu yeyote ambaye hakuwa na hatia, hivyo walidhani kwamba Yesu alikuwa mharifu.

Njia pekee ya Pilato kumhukumu Yesu palipaswa pasiwepo na chaguo lingine. Njia pekee ya Viongozi wa Kiyahudi kufanikiwa katika kumuua Yesu ilikuwa ni kwamba Yesu apelekwe kwao kwa njia ya kunyemelea (kwa siri) ili waweze kumhumu Yesu kwa siri bila ya mkutano kujua, mpata itakapokuwa baadaye. Kwa nini? Makutano walimpa Yesu! Yesu aliponya waongonjwa. Yesu alifufua watu waliokufa!

Kifo chake kilitakiwa kiwe maalum, kilitakiwa kitabiriwe na unabii wote ulitimia katika kila njia. Mungu alijua kwamba muda wa utawala wa Kirumi, na muda wa Pilato, Kayafa, Herode, na Yuda Iskariote ndio uliokuwa muda unaofaa kwa kufanikiwa kwa ajili ya dhabihu kuu iliyo fanywa. Mungu alijua tangu mwanzo, na hakufanya mtu yeyote afanye maovu. Mungu alijua nini watu wale waangechagua, kwa sababu Mungu anaweza kuona mambo ya ujao. Mungu aliweza kuona kwamba wakati huyo ilikuwa wakati bora kwa ajili ya kupata wokovu wanadamu kutoka kwenye uharebifu wa milele. Msaliti alikuwa ndiye njia pekee kwa ajili ya viongozi kufanikisha mipango yao mibaya, na Mungu alifahamu hili.

Unabii. Katika Zaburi 41:9, Mungu alisema kwamba rafiki mwema ndiye atakayekuwa msaliti, siyo adui. Katika Zekaria 11:13, Mungu alisema kwamba bei itakuwa vipande 30 vya fedha, ambavyo pia vitanunua konde la mfinyanzi. Viongozi wa Kiyahudi waliyafahamu maandiko yote juu ya Masihi, lakini walifanya mipango yao binafsi. Pesa, utawala, na umaarufu ni vihamasishaji vya nguvu katika maovu, bila kujali maarifa. Maarifa yanasukumwa pembeni tunapotamaani fedha, utawala au umaarufu.

Usaliti maana yake nini? Maana yake si uaminifu, udanganyifu, unafiki, ukafiri, na uwongo. Kumsaliti mtu, maana yake ni kwamba kwanza unatakiwa kuwa rafiki yake wa kuaminika. Unatakiwa kuwa rafiki yake kwa muda mrefu, na unahitaji upendano wako ni uwe wa kuweza kuthibitika. Ni lazima uwe na sababu ya kumsaliti rafiki. Kupenda pesa, nguvu au umaarufu au chuki ya ghafula kwa rafiki. Basi, ni lazima utafute maadui wa rafiki, maadui watakaokuwa tayari kumwangamiza mtu fulani. Maadui wengi hawaangemwanagamiza mtu fulani, lakini wachache...ndio. Baada ya kutafuta maadui wabaya, ni lazima unaonana nao, unaongea nao, unatumia muda wasirini pamoja nao. Unahitaji kupata tumaini la maadui kwa muda mrefu na kuwaambia kwamba unaweza kumleta rafiki yako mikononi mwao kwa bei uliochagua ambayo ni nzuri. Ni lazima mnafanye njama pamoja nao, mnajadili siri za rafiki yako pamoja nao. Mnakubaliana juu ya bei ya kusaliti na kuikubali. Matendo 1:15-17.

Yuda alimpa Yesu. Hakumchukia rafiki yake. Yuda alifikiri yeye ni rafiki mzuri. Mungu alisema kwamba rafiki atamsaliti Yesu, siyo adui. Je, shida ya Yuda alikuwa nini? Alipenda pesa. Tunajua hivi tunaposoma Yoh. 12:1-8. Yuda alipenda pesa zaidi ya ukweli, na zaidi ya upendo, na zaidi ya uaminifu, na alipenda pesa zaidi ya kuenda mbinguni. Alipenda pesa yote, pia shilingi chache tu! Hakuhitaji kuwa na mamilioni ya shilingi, lakini shilingi moja tu ilikuwa inatosha.

Yuda alijua kwamba Yesu alikuwa mfalme (Mathayo 16:16-19), na Yuda aliamini kwamba Israel ni ufalme wake. Yuda alikuwa mmoja wa mitume wa Yesu, na labda alifikiri kwamba yeye ni rafiki wa mfalme angeweza kuwa na pesa nyingi! Yuda alitaka Yesu kuwa mfalme haraka kwa sababu Yuda alitaka kuwa tajiri haraka. Hakupenda kusubiri muda zaidi. Alichagua kwa kumsaidia Yesu kuonesha mamlaka yake haraka ili Yuda aweze kutengeneza pesa! Labda alifikiri kwamba Yesu angepigana vita juu ya Warumi, na Waisraeli watawashinda Warumi. Sababu yoyote aliokuwa nayo Yuda, alisahau kuwa rafiki wa kweli.

Yuda alikuenda mbele ya viongozi wa Kiyahudi, maadui wa Yesu. Yuda aliongea, na alikubali juu ya vipande 30 vya fedha, ambayo ndiyo ilikuwa bei ya mtumwa! Mtumwa? Tusome Kutoka 21:32.

Kwa nini hakutaka zaidi? Yuda alimpenda Yesu, lakini alifikiri kwamba Yesu hakuwa na thamani zaidi ya mtumwa!

Vipi kuhusu sisi leo?

Ilituweze kumsaliti Yesu leo ni lazima tumfahamu kwanza, tutembe naye, tuongee naye, na kufanya kazi naye. Ni namna gani tunavyoweza kumsaliti leo?

1. Wakristo wengi leo wanamsaliti kwa kumuua kwa vitu...kama pombe.
2. Wakristo wengi wanamsaliti kwa kuuza urafiki wake kwa kuongopa, kuiba, kuzini.
3. Wengi wanamuua Yesu kwa kuwa na nguvu katika jamii, au kazi nzuri.
4. Wengine watamuua Yesu kwa sababu ya mashamba yao.
5. Wengine watamuua Yesu kwa sababu ya kutembelewa na familia au marafiki.

Wote tumewahi kumsaliti Yesu kwa namna moja au nyingine. Bei yako ilikuwa kiasi gani? Utamuua Yesu kwa ajili ya kitu gani? Bei ya kusaliti hivi, punde au baadaye, itathibitisha kuwa ya muda mfupi tu na itatoweka. Math. 16:26

Yuda alikuwa na nafasi ya kutubu. Badala yake aliamua kujinyonga na kupoteza roho yake. Matendo 1:15-20.

Tunapomsaliti Yesu leo, pia nasi tuna nafasi ya kutubu, 2 Kor. 7:9-10.

Usiwe kama Yuda umsaliti rafiki yako mwema Yesu. Yoh. 15:13-14.

Kama ukifanya hivyo: tubu na kubadilisha maisha yako, rejea tena kwa Yesu atakukamilisha tena. Usijinyonge; uwe kama Paulo aliyebadilisha maisha yake kwa ajili ya Kristo. 1 Tim. 1:12-17.

Ni lazima kukumbuka kwamba kumsaliti Yesu, maana yake kwanza unatakiwa kuwa rafiki yake wa kuaminika. Je, ni wewe rafiki wa Yesu? Kwa ajili ya kuwa rafiki wa Yesu ni lazima kumtii. Yesu alisema sisi ni lazima tumwaamini, na tubaptizwe, na tuendele katika matendo mema. Tena, je, ni wewe rafiki wa Yesu? Je, unamsaliti Yesu? Unaweza kutubu hivi leo! Kuacha tuama yako! Kuacha dhambi. Kugeuka na kuanza kufanya haki na mema. Kwa kuanza tena kumpenda Yesu zaidi ya mambo. Ufunuo 2:4-5.

Kuziko

Math. 27:57-61; Lk. 23:50-55; Yoh. 19:38-42

- I. Yesu alisulibiwa, alikufa na alizikwa. Kuzikwa maana yake nini?
- A. Kukizika kitu fulani ni kukiondoa kisionekane, kwa kawaida ni ndani ya ardhi au katika sehemu ambayo hakika itakuwa ni vigumu kukirudisha tena.
 - B. Tunazika watu kwa sababu wamekufa.
 - C. Kila nchi ina njia yao ya kushughulika na wafu.
 - 1. Nchi zingine wanachama maiti mpaka wawe majivu.
 - 2. Wengine wanachima mashimo marefu ardhini, wanaufunga mwili kwenye nguo au kwenye sanduku, na kuuweka shimoni na kuufukia kwa udongo.
 - 3. Wengine wanachimba mapango katika pande za milima na kutengeneza “matuta” kutoka kwenye kuta ili waweke miili mingi ndani yake.
 - a. Mapango haya kwa kawaida huwa kwa ajili ya familia nzima, wanayatumia kwa kuongeza miili hiyo kwa miaka mingi.
 - b. Mawe makubwa yana viringishwa kufunika mlango wa pango, na mawe haya ili ya viringishwe yanahitaji wanaume wengi ili mwili mpya uweze kuingizwa pangoni.
 - i. Hili ndilo aina ya kaburi ambalo Yesu alizikwa.
 - 4. Wengine wanajenga majengo ya mawe (yanakuwa makubwa kama mapiramidi ya misri au madogo kama nyumba), ya kiwa na milango mizito ya mawe au chuma, na wanatengeneza “matuta” ya mawe kwa ndani kwa ajili ya nzima zitakazo lazwa humo kwa miaka mingi.
- II. Kwa nini tunazika, au kuficha, maiti?
- A. Kwa sababu wanaanza kuoza.
 - 1. Wanaanza kumeguka na kunuka vibaya sana.
 - B. Tunapokuwa tumebatizwa, tunafananishwa na kifo na mazishi ya Yesu kwa njia rahisi.
 - 1. Tunapofufuka kutoka majini, kuna kitu kinacho takiwa kuachwa nyuma yetu ndani ya maji!
 - a. Maiti
 - b. Mwili wa dhambi na mauti ni lazima vibaki majini (kaburi). Rum. 6:11.
 - 2. Tumekufa katika dhambi na kuwa hai kwa Kristo.
 - C. Dhambi ndiyo iliyokaburini na dhambi ni mbaya inanuka kama maiti, mwili unaoza.
 - 1. Yak. 2:26—Mwili pasipo roho umekufa.
 - a. Tunapotoka majini tunakuwa roho, na tunatakiwa kuishi kiroho, tukitazamia mbinguni na kutenda matendo ya haki.
 - b. Kwa hiyo, mwili wa dhambi na kifo ni lazima ubakie katika hali ya kuzikwa kwa sababu ni mbaya na unanuka vibaya sana.
 - 2. Kol. 2:11—Tunatakiwa kuuvua mwili wenye tamaa za kimwili na kuuweka mbali!
 - 3. Kol. 3:1-4—Akili zetu tuziweke takia mambo ya mbinguni na wala siyo katika tamaa za mambo ya mwili (Gal. 5:16-26).
 - 4. 1 Kor. 15:42-49—Mwili wa asili hautaingia kamwe mbinguni.
 - a. Ila tu mwili wa rohoni, uliomtii kwa Mungu, utaweza kuiona mbinguni.
 - b. Usifikiri hata kidogo juu ya kuufukua mwili wako wa zamani wa dhambi.
- III. Tunapokuwa tumeuzika mwili wetu wa zamani wenye dhambi, tunatakiwa kuchuchumilia mbinguni (Filip. 3:4).
- A. Tatutakiwa kutazama nyuma.
 - B. Tatutakiwi kuanza kufikiri juu ya kufukua maiti zetu (Lk. 9:62).
 - 1. Tunapotazama nyuma, tukitamani mwili wa maisha yetu ya dhambi hatufai katika ufalme wa Mungu. Tubu!

C. Tunapokuwa tumebatizwa, tunakuwa tumeoshwa na kusafishwa (Mdo. 2:38).

1. Tunapoanza kufanya dhambi, tunakuwa tumefukua miili yetu ya zamani na kuivaa tena!
 - a. Mwili huo umeoza, unanuka vibaya na ni mbaya.
 - b. Maana yake wewe ni mbaya sawa na wengine wote ondoka kwa Mungu na Kristo! Ufu. 3:15-16.
 - c. Mungu hataruhusu mili iliyooza kuingia mbinguni.
2. Unapoamua kuiba, kuzini nje ya ndoa, kumtendea mme wako maovu, kuwapuuza watoto wako, au kuacha kukusanyika na watakatifu kwa ajili ya sababu za kidunia, hapo unakuwa umeuvaa ule mzoga.
 - a. Unakuwa kinyaa mbele za macho ya Mungu. Unakuwa kama matapishi! (2 Pet. 2:20-22).
 - b. Mungu hawezi kumwona Yesu amevaliwa wewe (Gal. 3:27).

IV. Unapokuwa umebatizwa, unaongezwa katika kanisa. Kanisa ni bibi arusi wa Kristo (Efe. 5).

A. Mabibi arusi wakati wote wanaonekana wasafi wamevaa vizuri, wakijiandaa kuolewa, siyo?

1. Wakristo wanaorudi katika dhambi hawaonekani tena kama mabibi arusi!
2. Hakuna mtu ambaye anapenda kumwoa mtu ambaye amevaa vizuri katika maiti iliyo oza.
 - a. Nijambo ambalo halifikiriki!

V. Iache maiti kaburini. Enenda katika Kristo.

A. Mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa yeye aliyewaita muishi katika nuru (Kol. 1:10).

Kukana

Mat. 26:69-75; Luka 22:54-62

I. Neno kukana linamaana gani?

A. Kwenye kamuji:

1. Ni kule kukataa kutimiza ombi au matakwa .
2. Ni kule kukataa kukiri ukweli au kumjua mtu au kitu.
3. Kupinga (kusema hapana juu ya mtu au kitu fulani).

II. Kila mtu hukana mtu fulani au kitu fulani kila siku.

A. Wakati mwingine hilo ni jambo lililo jema.

1. Tunawanyima watoto wetu haki ya kucheza barabarani kwa sababu watakufa.
2. Tunajinyima haki ya starehe fulani ili tuweze kuwa na chakula.
3. Tunawanyima watu wavivu pesa zetu kwa sababu wanatakiwa kufanya kazi ili kupata chakula (2 Thes. 3:10).

B. Wakati mwingi hilo ni jambo baya.

1. Tunaweza kukataa ukweli wa dhambi maishani mwetu.
2. Tunaweza kupinga dhambi ilipo kwenye maisha ya wale tunaowapenda.
3. Tunaweza kukataa kwamba mtu fulani tunamjua.

C. Sisi sote kwa wakati mmoja au mwingine tumekataa kumjua Kristo kama Petro alivyofanya siku Yesu alipokufa.

1. Petro alikuwa ameahidi kwamba hatomwacha Yesu.
2. Alikuwa amamfuata Yesu na waliomkamata, pengine alikuwa akitafuta njia ya kumwokoza rafiki yake.
3. Alitangatanga akiwa miongoni mwa askari na watumishi wa baraza la Wayahudi waliokuwa maadui wa Kristo, akisubiri ufuke wakati wa kumuonyesha Yesu jinsi alivyokuwa mwaminifu.
4. Alikuwa anajificha pekee yake kati ya maadui wa Kristo.

D. Petro akamatwa—kama inavyotutokea na sisi wakati fulani.

1. Mtu aligundua mazungumzo yake wakati anataka ampita adui mmoja wa Kristo
 - a. “Ulikuwa pamoja na Yesu wa Galilaya!”
2. Petro akiwa amesimama katikati ya kambi la maadui msichana anatoa kwa sauti kubwa hilo tangazo.
 - b. Petro ilimubidi ajitete la sivyo asingepata nafasi ya kumwokoza Yesu! Angewezaje kumsaidia Yesu kama yeye mwenyewe angekuwa gerezani.
3. Baadae, msichana mwingine akamgundua na kwa sauti ya juu akatoa hilo tangazo kwamba Petro alikuwa ni mfuasi wa Yesu.
 - a. Kwa sauti ya juu tena, Petro akamjibu kwamba alikuwa amekosea!

4. Kunapokaribia kupambazuka, baadhi ya watu walikuwa wanamwangalia Petro halafu wakasema kwamba kwa hakika alikuwa ni rafiki wa Yesu.

- a. Petro alikuwa amechoka na akawathibitishia kwamba yeye hakuwa rafiki wa Yesu kwa kutumia lugha mbaya au kwa kuapa.
- a. Hakutaka asimame aonekane kuwa yupo tofauti na umati wa watu alitaka kujicha nganya.

III. Jogoo akawika

- A. Kuwika kwa jogoo kulileta maana kwa Petro tu na si kwa mtu mwingine.
 - 1. Yesu alimwambia hapo mwanzo ni kwamba kabla jogoo hajawika Petro atakuwa amemkana Yesu mara tatu.
 - 2. Katika Luka 22:61, panasema kwamba baada ya jogoo kuwika, Yesu alikuwa karibu, akageuka kumwalia Petro.
 - a. Ni lazima tukumbuke kwamba Yesu siku zote yupo karibu, na anajua tunapomkana.
 - b. Petro alilia kwa uchungu.
 - 3. Wakati anajaribu kumsaidia rafiki yake mpendwa, Yesu, Petro alikuwa amemwangusha Yesu kwa namna mbaya kabisa.

IV. Hii ilitokeaje?

- A. Huwezi kujificha kuhusu kuwa Mkristo.
 - 1. Anayemfuata Kristo huongea, huvaa na mitenda tofauti.
 - a. Mazungumzo: Efe. 4:25; Efe. 5:4; Mt. 12:34-37
 - b. Kuvaa: 1 Tim. 2:8-10
 - c. Matendo: Mt. 5:16; Efe 6:5-9; 1 Kor. 15:58; Kol. 3:17
 - 2. Mtu anayemfuata Kristo ana mwanga tofauti ndani yake.
 - a. Mt. 5:4-16—tunachokifanya kinaweza kuonekana kuwa ni chema siyo kiovu.
- B. Unapokuwa pamoja na maadui wa Kristo watakutambua tu.
- C. Kwa kawaida hofu ndiyo husababisha tumkane Kristo.
 - 1. Hofu ya kufa, maumivu, au kupuuzwa na watu.
 - 2. Hofu ya kumpoteza mtu unayempenda au kumheshimu.
 - 3. Hofu ya kupoteza kitu unachodhani unakihitaji.
 - 4. Hofu ya kuwa peke yako tu unayeamini na kutii neno la Mungu.

V. Yesu alisema kuwa kama tutamkana basi naye atatukana mbele ya Mungu siku ya mwisho. Mt. 10:33

- A. Tapokuwa huwa anatupatia nafasi ya kuhuzunika na kubadilika, kama alivyomfanyia Petro.
- B. Tunapotubu hatubaki peke yetu, ni lazima turudi kwa wafuasi wengine wa Kristo.
 - 1. Kwa ajili ya hamasa na kuonya majeraha ya roho.
 - 2. Kuwahasisha wengine ili waondokane na hofu.
- C. Yesu alisema katika 1 Kor. 15:33, tunapokuwa na ushirika na watu waovu wanaweza kutuvuta mpaka tukamkana Kristo, au kumwacha Kristo ili kutenda dhambi.
- D. Yesu alisema katika Mt. 16:24, kwamba kama tutakana jambo lolote, basi ni muhimu tukajikana wenyewe.
 - 1. Kukataa tamaa zetu za kimwili, kiburi cha uzima na tamaa za macho (1Yoh. 2:16).
 - 2. Tunatakiwa kiwikana vitu hivi kwa sababu tunamwogopa Mungu na tunauogopa moto wa milele wa jehanam.
 - 3. Rum. 6:13—tunapaswa kuitoa miili yetu, na sisi wenyewe kama silaha za haki kwa Mungu.
 - a. Maana yake tujiweke kimwili mbele ya Mungu na kujiweka tayari kwa kazi njema machoni pa Mungu
- b. Tunapojiweka mbele ya maadui wa Mungu mambo yanaweza kuwa

mabaya

- E. Tukilazimishwa kuwa mbele ya maadui (kutokana na vita au kutekwa nyara), tufanye nini?
1. Hatutakiwi kuogopa, hatutakiwi kumkana Kristo.
 2. Tunaweza kumkumbuka Petro na tatizo lake.
 3. Tunaweza kumkumbuka Danieli, Shadraka na Abedi-nego.
 - a. Walilazimishwa kusimama mbele ya maadui zao na walikutaa kumkana Mungu.
 4. Ni lazima tukumbuke Ufu. 2:10, pale Yesu anapowaambia kanisa wawe waaminifu hata mbele ya uso wa mauti, bila kiyali kinachotokea au nani yuko kando yetu.
- F. Usimkatae Yesu, usikatae kwamba unamjua Yesu: uwe mwaminifu hata ukiwa na hofu.

Chaguo

Matt. 27:15-26

I. Kila siku tunafanya machaguo

- A. Machaguo ambayo hayana maana yoyote iliyo halisi kama vile tule nini, tuvae nini.
- B. Machaguo yanayo maanisha uzima na kifo cha kimwili, kama vile, kuvuka barabara bila kuwa mwangalifu.
- C. Machaguo yanayo maanisha uzima na kifo cha kiroho, kama vile nimwombe Mungu au nisimwombe.
- D. Machaguo yanayo tengeneza matakwa mema au mabaya.
- E. Machaguo yajengayo na machaguo yaharibuyo.

II. Neno “chaguo” linamaanisha nini?

- A. Ni kuwa na zaidi ya kitu kimoja cha kufanya na tunachagua, chagua au chukua kimoja kati ya vitu hivyo.
 - 1. Kwa mfano, kama tunataka kwenda Dar, tunaweza kuchagua kama tutakwenda kwa njia ya mzunguko au kuwa njia ya mkato, tunaweza kuchagua basi la gharama, ndege au kutembea kwa miguu.
- B. Mungu ametupatia mifano mingi kwenye Biblia ya watu waliofanya machaguo.
 - 1. Hawa alichagua kifo badala ya uzima.
 - 2. Adamu alichagua kumfuata Hawa wakati hakutakiwa.
 - 3. Nuhu alichagua kutengeneza safina na kuingia ndani yake, ulimwengu mzima ulichagua kutofanya hivyo.
 - 4. Yakobo alimfuata Mungu baada tu, alipofanya kila machaguo mabaya katika maisha.
 - 5. Daudi alichagua kuwa mwema na Sauli hakuchagua hivyo.

III. Chaguo kubwa kuliko yote ulimwenguni (Mat. 27:15-26).

- A. Ilikuwa ni siku ya kuwasulibisha waharifu watatu, na viongozi wa kiyahudi walitaka Yesu awe mmoja wao.
 - 1. Pilato alijua kwamba Yesu hakuwa na hatia na hakutaka kumuua Yesu.
 - 2. Pilato alijua kwamba viongozi walitaka Yesu auawe kwa sababu ya husuda (Mat. 27:18).
- B. Pilato alimtoa kwa watu muuaji jina lake Baraba na aliwapatia chaguo: Yesu au Baraba.
 - 1. Baraba alileta kifo kwa watu
 - 2. Yesu alileta uzima kwa watu (Yoh. 10:10).
- C. Watu kwa sauti kuu, alichagua kifo kiishi na uzima ufe.
 - 1. Kwa nini walitaka kumuua mtu aliyefanya mema tu? Husuda.
 - a. Walionea wivu mamlaka yake, kufahamika kwake, na ukweli wa kwamba aliwafadhaisha wakati wote.
 - 2. Kwa nini mtu anachagua kuzini? Tamaa, kutamani, matakwa binafsi.
 - 3. Kwa nini mtu anataka kuchagua kuiba? Husuda, njaa, tama ya kutaka kutajirika haraka, au pengine wanawachukia wengine.
 - 4. Kwa nini anachagua kuongopa? Ili ajilinde mwenyewe, ili afiche kitu fulani, au kumchukia mtu fulani.
- D. Machaguo yote ambayo matokeo yake ni maumivu, kifo na balaa ni machaguo mabaya.
- E. Machaguo yote mabaya yanaongoza kwenye kifo na mateso (Rum. 6:23).

IV. Walipo mchagua Baraba, walichagua kifo.

- A. Baraba alikuwa muuaji.
- B. Kila siku tunatakiwa tujipime wenyewe, tuangalie kile tufanyacho, tuwazacho, na tuchaguacho.
 - 1. Tuamkapo tukiwa katika hali mbaya, tukisema maneno yenye hasira, yanayo wachukiza

wengine, tunakuwa tumechagua chaguo gani? Kifo.

2. Tumwonapo mwanaume mzuri akipita na kunajiruhusu kuwaka tama na kuwa jirani sana naye na kumkonyeza kwa macho yetu, tunakuwa tumechagua nini? Kifo.
 - a. Uzinzi na uasherati ni kifo.
3. Tunapofanya kazi na pesa katika vitengo vyetu vya kazi, na tunatamani kwamba baadhi ya kiasi cha fedha hiyo kingekuwa cha kwetu, na tunainyakua hiyo pesa na kuiweka kwenye mikoba yetu au mifukoni mwetu, tunakuwa tumechagua nini? Kifo.

- C. Tunapochagua kitu fulani, machaguo mengine yote ya nasukumwa pembeni! Tumemchagua Baraba! Yesu anasukumwa na kuwekwa pembeni na tunakuwa marafiki wa Baraba.
1. Efe. 2:1-2—Pasipo Kristo kifo tu ndicho kipo. Kuwapo pamoja na Kristo kuna uzima.
 2. Rum. 6:11—Kama tutachagua kifo, tuchague kifo kilicho sahihi.
 - a. Kifo cha dhambi na maovu ni kifo kisicho na haki maishani mwetu!
 3. Rum. 6:12-13—Tunapovitumia viungo vyetu vya mwili kufanya mambo maovu, Mungu atatuangamiza.

V. Baada ya ufufuo ya Yesu, Yesu aliwapatia watu chaguo sawa sawa na chaguo ambalo Pilato aliwapatia makutano waliokuwa na hasira.

- A. Marko 16:15,16—Aliwaambia amini na kutii na upokee uzima, au usiamini na upokee kifo.
- B. Kumbuka, viongozwa kidini, watu wa Mungu, wasikuza Yesu walifanya chaguo la kutenda maovu.
 1. Kwa sababu tu tunahuduria ibada na uimbaji na kuomba na kushiriki meza ya Bwana haimaanishi kwamba hatutachagua kifo kwa wakati fulani (1 Kor. 10:12).
- C. Vipi kuhusu wewe? Ni nani ambaye unamchagua sasa? Yesu au Baraba? Uzima au Mauti?

Kuuliza

Math. 26:57-69; 27:11-14

I. Watu wengi katika Biblia wamemuuliza Mungu. Ni sawa tu kumuuliza Mungu swali, lakini ni njia nzuri na njia mbaya. (Mt. 7:8)

A. Mifano ni:

1. Kaini: “Kwani mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?” (Mwanzo 3)
 - a. Ni aina gani ya jibu Kaini alikuwa anahitaji? Hakuna. Alikuwa anaonyesha. maonyesho ya kutokujali na ujasiri kwa kumjibu Mungu jeuri. Mungu alimwadhibu.
 2. Farao: “Mungu ni nani ambapo ni lazima nimsikilize?” (Kut. 5:2)
 - a. Ni aina gani ya jibu Farao alikuwa anatafuta? Hakuna. Alikuwa anajivuna. Mungu alimwadhibu.
 3. Gideoni: “Kwa nini mateso haya yote yametupata sisi? Iko wapi miujiza yote ambayo baba zetu waliona? Mimi nitawezaje kuwaokoa watu wa Israeli?”
 - a. Alitaka kuyabadili maisha yake yote moja kwa moja. Mungu alimbariki.
- B. Mungu anasema kwenye Isaya 1:18, tunaweza kuja kwake na kusemezana.
1. Yohana 10:10—Tukiishi jinsi Mungu anavyotaka tutakuwa na uzima tele.
 - a. Ni lazima tuulize maswali ilikiyiboresha siyo kama yale ya Kaini na Farao.

II. Yesu

- A. Wanafunzi: Mt. 26:20-25—Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba mmoja wao atamsaliti
1. Wote waliuliza swali: “Ni mimi Bwana?”
 - a. Hakuna hata mmoja wao aliyeelewa jibu la Yesu la moja kwa moja.
 - b. Wakati fulani tunauliza maswali kwa nia njema na tunashindwa kuona au kuelewa jibu.
- B. Kuhani Mkuu: Mt. 26:62, 67, 68—Kuhani mkuu aliuliza baadhi ya maswali:
1. “Hunijibu?” Kuhani alita Yesu auawe.
 2. “Ni nini jambo hili ambalo hawa watu wanakushtaki kwalo?” Kwa mara nyingine alitaka kumtegea Yesu.
 3. Yoh. 18:19-20—Kuhani mkuu aliulizia kuhusu mafundisho ya Yesu na jawabu la Yesu lilikuwa ni kukemea, kwa sababu kuhani mkuu alijua kila kitu kuhusu mafundisho ya Yesu kwa kuwa Yesu hakufundisha kwa siri.
 4. Walinzi na makuhani wengine walimchapa Yesu makoti:
 - a. “Ni nani amekupiga?” Swali lao lilikuwa ni kutaka kujifurahisha na kumuumiza.
- C. Pilato: Mt. 27:11-13; Yoh. 18:35, 38; Yoh. 19:10
1. “Hausikii jinsi yalivyo mengi mambo wanayokushtaki?” Pilato alikuwa anapoteza muda wake.
 2. “Je, mimi ni Myahudi?” Alitukana kama Kaini alivyouliza swali, Pilato alikuwa anajitafutia ujasiri.
 3. “Umekosa nini?” Yesu alimpa jibu refu sana lakini Pilato alikuwa hasikilizi.
 4. “Je, wewe ni mfalme wa Wayahudi?” Jibu la Yesu halikujalisha.
 5. “Kweli nini?”
 - a. Swali muhimu kama hilo, lakini Pilato hakusubiri jibu. Yesu hakujaribu kumjibu. Pilato akajua kwamba amekosea ila hakutaka kufanya mabadiliko akanawa mikono yake
 6. “Haujuwi kwamba naweza nikakufungulia?” Jibu la swali hilo lilikuwa Mungu ndiye aliyempa uwezo huo Pilato.
 7. “Huzungumzi nami?” Pilato alikuwa amechukia.
 - a. Alitaka Yesu ajitetee lakini Yesu hakuhitaji. Hakuwa na hatia na wote walijua. Pilato angeweza kumwachia Yesu muda ule ule anapofika.

III. Ukiwa na Mungu wa ulimwengu mikononi mwako.

- A. Makuhani walikuwa na Mungu wa ulimwengu kimwili mikononi. Maswali mengi waliyouliza yalikuwa ya kijinga, ya kiburi na ya matusi.
1. Leo hii mimi na wewe tuna Mungu wa ulimwengu mikononi, maneno yake yako kwenye Biblia, tuna zaidi ya miaka elfu nne ya majibu kwenye Biblia (1 Pet.:3, 4). Ni aina gani ya mswali tunayomuuliza Mungu leo? Ni lazima tutafute majibu aliyokwisha kutupatia na sio kuleta mchezo.
 2. Wanafunzi wa Yesu waliuliza maswali muda wote wakayageuza maisha yao kufanana na Yesu.
 3. Siyo vibaya kumuuliza maswali Mungu lakini kibaya ni msukumo wa swali na ndio utakaoamua mwitikio wetu kwenye yale majibu
 4. Ni aina gani ya maswali unauliza? Na unasukumwa na nini ili uulize swali? Mwitikio wako ni nini?
4. Je, unaitikia kama Makuhani wa Yahudi waliomhukumu Yesu? Je, unaitikia kama walenzi waliompiga? Je, unaitikia kama Pilato aliyenawa mikono? Au, je, unaitikia kama wanafunzi wake waliobadili maisha yao vyema?

Kusulibishwa

Mat. 27:31-50; Yohana 19:31-37

Kusulibishwa maana yake, ni kumweka mtu juu ya msalaba ili afe kwa maumivu ya siyo na kifani. Msalaba ulitengenezwa na Waajemi wa zamani kama nguzo ya mti ambayo walikuwa wanamning'iniza mtu kwa mikono toka juu na chini wanamfunga miguu yake. Mtu huyu alikuwa anakufa kwa njaa, kiu, au kwa wanyama pori na ndege. Baadaye, Warumi waliendeleza aina hii ya kifo kwa kuongeza ubao ili kwamba mharifu aweze kugawanywa, hii ilifanya awe na wakati mgumu wa kupumua, na waliongeza misumari mikononi na miguuni ili kuongeza mateso. Siyo hivyo tu. Kabla ya kusulibishwa walichapa mgongo wa mharifu ili watengeneze mateso makubwa alipokuwa msalabani.

Kuwauwa watu kwa kuwaweka misalabani ilikuwa ni kanuni ya Warumi ya adhabu kwa watumwa, wakiukaji na wavunjaji wa sheria ambao hawakuwa raia wa Rumi. Kilikuwa ni kifo cha maumivu makuu na uchungu walicho kitunga. Natujifunze aina hii ya adhabu kuu kwa kumwanguka ndugu yetu, Yesu.

Kabla ya kusulibishwa, Yesu alichapwa kwa mijeledi maalumu. Mijeledi ilikuwa na mipini mifupi ya mti. Kwenye ile mipini kulifungiwa kamba za ngozi mbili au zaidi. Mwishoni mwa kila kamba kulifungiwa vipande vya mifupa na chuma ambavyo vilijikita na kuchana nyama ya ngozi ya mwanadamu.

Yesu alifungwa akiwa uchi, juu ya nguzo ndefu mikono yake ilinyoshwa kuizunguka hiyo nguzo, ili kwamba mgongo wake uwe wazi. Mijeledi ilichana pande za mgongo wa Yesu kwa mfano wa mraba, kwa kwenda chini pande zote za mwili kuelekea uti wa mgongo. Mwili wa mfungwa ulikuwa unachanwa, na sehemu zilizochanwa ziliachwa zitoke damu nyingi sana.

Baada ya kuchapwa mijeledi, baadhi ya watu katili walitengeneza taji la miba na kulipachika kichwani pa Yesu! Majeraha ya kichwani yanamwaga damu nyingi sana, hata majeraha madogo. Hebu fikiri majeraha mengi kichwani pake, yote yanatoa damu bila kuzuiwa. Kwa wingi wa damu imwagikayo kwa mtu ndivyo awavyo dhaifu, kwa sababu uhai upo kwenye damu.

Maaskari wakamvalisha Yesu nguo zake tena na vazi lilikwama mwilini mwake kwa sababu ya damu. Damu ilikauka wakati walipofika kwenye sehemu ya kusulibishia. Warumi walichofanya ili kuongeza mateso kwa mfungwa, waliikandamiza boriti ya msalaba mabegani mwa mfungwa, na walifunga boriti nzito mikononi mwake ili ishikiliwe juu. Sasa Yesu alikokota mti huu mrefu, mzito kwenye mabega yake yaliyojeruhiwa, wakati uo huo mavazi yake nayo yanamkwaruza kwenye vidonda vyake vilivyo kauka. Yesu alilinyanyua hili boriti la msalaba, ambalo lilikuwa na uzito wa kilogramu 34 hadi 57 alifikishe hadi kwenye mlima wa mauaji nje ya mji. Yesu akadhooifika sana kwa sababu ya damu nyingi aliyomwaga, akaanguka chini. Maaskari waliamru mtu mwingine abebe msalaba kwa ajili ya Yesu.

Mtu yule alifikirije alipobeba msalaba wa Yesu huku maelfu ya watu wakizomea na kupiga kelele? Usingefikiri kwamba angetubu kama alikuwa mtenda dhambi na kuwa mtu mwema? Hata hivyo, hatujui.

Sehemu ile ya kifo, iliitwa Sehemu ya Fuvu, ncha ya msalaba ilikuwa tayari imesimikwa ardhini. Wazoefu wa historia wanafikiri kwamba Warumi, wakati wa Yesu, walitumia msalaba ya futi nane urefu. Wakati boriti ya msalaba wa Yesu inaondolewa na kushushwa ardhini, maaskari walichana mavazi ya Yesu na mavazi yakachubua tena vidonda, na akajisikia maumivu zaidi. Kisha Yesu akatupwa chini ardhini akaangukia mgongo wake uliiteswa juu ya boriti ya msalaba wake.

Watu wengi walimfuata katika Sehemu ya Fuvu, walikuwa wanacheka au kuangalia. Katika hawa watu alikuwepo mama yake, rafiki zake na Yohana. Mitume wengine walikuwa mbali, wanaangalia. Watu waliokuwa mbali sana waliweza kuona kusulibishwa. Kusulibishwa kulifanyika hadharani.

Warumi walichukua misumari ya chuma, yapata kama nchi sita urefu na upana kati ya sm 1, na waligongelea msumari katika kila kifundo cha mkono wake, mbele ya kiganja cha mkono wa Yesu, ili waishikilizie mikono ya Yesu juu ya boriti ya msalaba. Misumari ilitoboa mshipa mkuu wa fahamu (neva kuu), jambo ambalo lingesababisha maumivu makuu, yakipita mikononi hadi kwenye moyo. Misumari haikuvunja mfupa wowote wa mshipa.

Kisha maaskari wakainua boriti ya msalaba juu, wakimwinua Yesu kwa mikono yake, wakaunyanyua huo msalaba juu sana mpaka nchi ya juu zaidi ya msalaba wakaipachika. Mara wakayakunja magoti yake, wakaipandanisha miguu yake na wakagongelea msumari mrefu miguuni pake. Na msumari huo pia, haukuvunja mshipa wowote wala mfupa, bali uliweza kuvunja mshipa wa fahamu (neva kuu) mwingine mkuu unaozunguka kwenye miguu yote hadi mwili mzima, jambo hilo lingesababisha maumivu makali sana pia. Kwa namna hii, kwa kupitia mikono yake na miguu yake, kila mshipa wa fahamu (neva) mwilini mwake ungepata maumivu ya ajabu.

Yesu alipokuwa anakumbana na aina hii ya mateso mbali mbali, maaskari waligongelea ubao kichwani pake ukisema kwamba alikuwa mfalme wa Wayahudi kiliandikwa kwa lugha tatu: Kiebrania, Kilatini, na Kiyunani. Maaskari walikuwa wanawapatia kileo kikali waharifu, ili kiwasaidie kutuliza maumivu yao, lakini Yesu alikikataa. Kwa nini alikikataa? Kwa sababu siyo tu alikuwa anakufa. Alikuwa ni dhabihu kwa sababu alitakiwa apitie kila aina ya mateso na maumivu kabla hajafa, kwa sababu alikuwapo ili achukuwe nafasi yetu. Hakuwahi kufanya dhambi kamwe. Sisi tulikuwa watenda dhambi. Sisi ndio tulitakiwa tuteswe. Yesu alitaka tufahamu kwamba alikuwa msalabani kwa sababu moja tu: awe kwa niaba ya nafasi yetu ya maangamizi, ilituweze kuepuka. Tulipaswa tuone maangamizi katika aina yake ya uhalisi ili kwamba tuweze kushukuru kukwepa kwetu kuliko kukuu.

Yesu alipokuwa ananing'inia msalabani, nzi na wadudu wengine walijipatia chakula kwenye vidonda vyake, katika ngozi yake na uso wake, wala Yesu hakufanya lolote juu ya jambo hilo. Jua lilimwakia. Ndege walikuja na kuwala waharifu pia, hasa wakikaa baada ya siku moja au mbili. Waharifu msalabani waliishi kwa siku sita bila kupata chakula wala maji. Siku sita!

Ilikuvuta pumzi, Yesu alitakiwa ajivute kutoka kwenye mikono yake iliyogongelewa misumari, lakini ili kupumua, Yesu alijisukuma kutoka kwenye miguu yake iliyogongelewa misumari, ili aweze kujinyanyua. Kama asingejinyanyua, angeshindwa kupumua na angeanza kujinyonga. Alipokuwa anajiviringisha, vidonda

vyake vya mgongoni vilijikwaruza mtini. Pia alikuwa juu angani, mbele ya wote walioweza kuona, alianza kujikojolea na kujinyea. Hapakuwa na siri yoyote, isipokuwa tu, kitambaa kilichofungwa kiunoni mwake, ili kuficha sehemu zake za siri.

Yesu alikuwa msalabani kwanzia kati ya saa 3:00 asubuhi hadi saa 9:00 mchana. Kwa wakati huu alipokuwa msalabani aliona kila mtu aliyekuwa mbali mbele yake. Aliweza kuwasikia na kuwaona maaskari wakimghadhibisha na wakiyapigia kura mavazi yake. Aliweza kuwasikia na kuwaona makutano wa viongozi wa Kiyahudi wakimghadhibisha na kumcheka na kumwangalia katika kila hatua aliyoipitia, katika kila tetemeko la maumivu yake. Aliweza kumwona mama yake na rafiki zake wakiwa jirani pake na aliwasikia wakilia. Saa 6:00 mchana, jua lilitiwa giza ghafula. Katika nyaraka zote kwenye Biblia zinasema pakawa giza. Pakawa giza mpaka Yesu alipokufa.

Yesu alisema mara kadhaa akiwa msalabani. Aliweza kusema tu alipokuwa anapumua kwa kujinyanua mwenyewe kwa miguu yake. Kila neno lilitamkwa katika maumivu ya kusulibishwa. Moja ya mambo ya kwanza aliyoweza kusema lilikuwa, “Baba wasamehe kwa kuwa hawajui walitendalo.” Eee! Katikati ya maumivu makali kabisa, njaa, kiu na aibu, Yesu alimwomba Mungu atusamehe. Je! twaweza kufanya hivyo? Yesu anatutake tufanye hivyo katika Mathayo 5:43-48 na Warumi 12:14, 1 Petro 2:23. Yesu anapotuambia tuwabariki wanaotuudhi.

Kwa mara nyingine Yesu alipojinyanyua akamwambia mmoja wa wale waharifu aliyekuwa pembeni pake, “Hakika nakwambia leo hii utakuwa nami kuzimu.” Eee! Baraka nyingine inatolewa akiwa katika mateso.

Wakati mwingine alimwangalia mamaye aliyekuwa analia kwa kwikwi jirani pake, na akamwambia, “Mama mtazame mwanao.” Akamwangalia rafiki yake, Yohana na akamwambia, “Mtazame mama yako.” Bado hii ni zawadi nyingine iliyotolewa akiwa katika mateso.

Karibu na mwishoni mateso yalipokuwa yakutisha sana, alijiinua na kulia kwa sauti kuu, “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?” Wakati huu maaskari walitwaa sifongo wakamnyweshwa. Sifongo chungu ikamwagwa mwilini mwake, na kusababisha maumivu zaidi katika vidonda vyake.

Hatimaye saa 9:00 mchana, Yesu akajiinua na kusema, “Baba, naiweka roho yangu mikononi mwako! Baba, naiweka roho yangu mikononi mwako.

Baadaye kidogo, alisema kwa sauti kubwa, “Imekwisha!”

Yesu alikufa. Wakati huu nchi ikatetemeka, pazia la hekaluni lililosimama kati ya Mungu na mwanadamu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini, na jua likachomoza tena. Yesu alipokufa, Mungu mwenyewe akawa anapatikana kwa wanadamu.

Baadaye viongozi wa Kiyahudi waliomba kwamba waharifu waliosulibishwa wangeshushwa na kuuawa mapema kabla ya giza la jioni (utusitusi). Katika siku hiyo, katika giza la jioni (utusitusi), siku kuu ya Pasaka ingeanza, siku ya kukumbuka kupona kwa Waisraeli toka kifoni kule Misri kwa damu ya wanakondoo. Viongozi hawa wa Kiyahudi walikuwa wajinga wa kuhuzunisha, kwamba walikuwa wamemchinga Mwanakondoo halisi. Warumi waliwavunja miguu wale waharifu, waliokuwa pembeni pa Yesu. Kwa kuwavunja miguu maana yake wasingeweza kujinyanyua ili wapumue, hivyo walikufa kwa kukosa hewa.

Wale maaskari walipomjia Yesu waliona kwamba alikuwa hapumui. Kwa kuwa hakuna mtu aliyeshushwa msalabani akiwa hai, walihakikisha kwamba alikufa kwa kumchoma mkuki ubavuni mwake. Maji na damu vikatoka kutoka kwenye shimo hilo ubavuni mwake. Tunapokufa, maji katika damu yetu yanajitenga na seli za damu. Yesu alikuwa amefariki muda mrefu wa kutosha ili hatua hii ifanyike.

Maaskari waliushusha mwili wake toka msalabani, kwa ukatili wakachomoa misumari iliyogongelewa mikononi mwake na miguuni mwake. Marafiki wa Yesu pamoja na mama yake wakaufunga mwili wake katika sanda na kuupake mafuta ya kuzikia na kuubeba mpaka kwenye kaburi la tajiri. Kiongozi wa maaskari alijua kwamba Yesu alikuwa tofauti. Alijua kwamba Yesu hakuwa na hatia. Baada ya kumtazama Yesu akipigwa mijeledi na kuenda katika Sehemu ya Fuvu la binadamu, na kuvumilia masaa sita ya mateso, na kisha kuwasamehe wauaji wake, yule kiongozi wa maaskari asingejiokoa mwenyewe. Alisema kwa ushuhuda mkuu, “Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu.” Unafikirije? Je, unaamini? Je, matendo yako na maneno yako ya kila siku yanathibitisha kwamba unaamini? Je, utafanya kama Yesu anavyoamuru na kuchukua msalaba wako kwa kumfuata? Je, utafisha tamaa zako mbovu msalabani?

Natuweke roho zetu mikononi mwa Mungu na tuishi kwa ajili ya Yesu...aliyetufia.
(Zaburi 22:1, 6-7, 11-21; Isaya 53:3-12)

Kifo

Math. 27:45-54

(1 Pet. 2:24—Yesu alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki)

I. “Sasa imekwisha.”

- A. Baada ya masaa 6 ya mateso mabaya juu ya msalaba, mbali na usiku mzima na asubuhi ya kuchapwa, kupigwa makofi, kupigwa ngumi, kutemewa mate, hatimaye kugongomewa—Yesu akafa.
- B. Yesu aliikabidhi roho yake kwa Mungu, alitoa roho yake, aliiacha itoke mwilini mwake.
 - 1. Yesu ndiye aliyetoa roho yake...msalaba haukuchukua uhai wake, Warumi hawakuchukua uhai wake, na wala Wayahudi hawakuchukua uhai wake.
 - 2. Yesu ndiye Bwana wa Uzima na Kifo (Yoh. 11:25).

II. Math. 16:24—Tunapaswa kuibeba misalaba yetu na kumfuata.

- A. Ni lazima tumfuate kimfano kwenye mlima wa Golgotha na tujiruhusu kusulibishwa na Yesu!
 - 1. Maana yake ni kwamba ni lazima tufe (Luka 9:23).
 - 2. Ni lazima tuinamie msalaba, tukielekea kifoni kila siku.
- B. Kol. 3:3—Tumekufa na tumefichwa ndani ya Kristo.
- C. Math. 10:38—Yesu anasema kwamba tusipofanya hivyo hatumstahili.

III. Rum. 8:13—Kama tunaishi kwa roho, kama tunamfuate Yesu, tunatakiwa tuyafishe matendo ya kimwili.

- A. Dhambi inatakiwa ifishewe.
- B. Yesu alikufa msalabani ili aweze kuwangamiza dhambi na matendo ya Shetani.
- C. Alikufa ili tuweze kusamehewa ili tuwe na maisha mapya.
- D. Ilikwamba tuweze kusamehewa ni lazima tufie dhambi kama yeye mwenyewe alivyofanya, ila tu siyo katika msalaba halisi.
 - 1. Rum. 12:1-2—Tunapaswa kuishi kwa ajili ya Yesu na haki, na kufa kwa ajili ya dhambi.
 - 2. Tunatakiwa luzamishwe maji, ni kwa ajili ya dhambi zetu (Mdo. 2:38).
- E. Rum. 6:4-5—Kuzamishwa majini, maana yake tumekuwa kama Yesu katika mauti yake.
 - 1. Tunapotoka majini kunafananishwa na Yesu katika ufufuo wake.
 - 2. Baada ya hapo ni lazima tuhakikishe kwamba tunabakia kuwa wafu katika dhambi...
 - a. Kwa kuuweka msalaba akilini mwetu kila siku.
- F. Filip. 3:10—Tunatakiwa tufananishwe na kifo chake, tubakie wafu katika dhambi.
- G. Gal. 6:14—Ulimwengu umesulibishwa kwetu.
 - 1. Kama tunaendelea kutenda dhambi, kifo cha Yesu na mateso yake vilikuwa ni kupoteza muda tu.

IV. Yoh. 15:13—Yesu aliwaambia wafuasi wake kwamba hakuna upendo mkuu kama wa mtu kutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake.

- A. Yesu alikufa kwa ajili yetu ili kwamba tuweze kuwa na uzima wa milele pamoja naye.
 - 1. Yeye ni rafiki yetu.
 - 2. Tunatakiwa tuwe rafiki zake, na tufe katika dhambi kwa kuheshimu upendo wake mkuu kwetu.
- B. Tukifa katika dhambi na uovu, tunathibitisha kwamba sisi ni rafiki zake.
- C. Yesu anapotwambia kwamba kila siku tujitwike msalaba wetu na kumfuata hiyo amri.
- D. Yoh. 15:14—Tunakuwa rafiki zake tukifanya atuamruyo.
- E. Rum. 6:10—Yesu ni mfano wetu jinsi ya kufa kwenye dhambi na kuishi kwenye haki.
 - 1. 1 Kor. 15:31—Paulo anasema jambo hili linawezekana, na yeye mwenyewe alikufa kila siku.
 - 2. Kufa kwa ajili ya dhambi kumefanywa na mamilioni ya watu tangia siku za Yesu. Inawezekana!

V. Kumfuate Yesu maana yake kufuata nyayo zake. Alikwenda wapi?

- A. Alikwenda katika sehemu mbali mbali kuhubiri neno la Mungu, akiwaambia watu kwamba walitakiwa kubadilisha maisha yao na kuanza kumpendeza Mungu.

- B. Alikwenda sehemu mbali mbali kumwomba Mungu.
- C. Alikwenda kwenye milima wa kifo na kufa msalabani, na kumwaga damu yake kwa niaba yetu, ili atupatie uzima.
- D. Kisha alifufuka na sasa anatembea na Mungu mwenyewe.
 - 1. Ebr. 12:12—Yesu aliuvumilia msalaba, na akaidharau aibu yake, aibu ya kufa kwa ajili ya dhambi na baadaye alikwenda kuishi mbele za uwepo wa Mungu.
 - 2. Filip. 2:8—Alikuwa mtii kwa Mungu.
- E. Yesu alitii, na sasa anatutaka tufanye vivyo hivyo.
 - 1. Kuyaacha maisha yetu ya dhambi inaweza kuwa jambo la kuumiza na kushangaza.
 - a. Maana yake tutapoteza marafiki zetu wa zamani, na wakati mwingine hata familia zetu, tunapoteza maisha yetu ya zamani na tunatakiwa kuanza maisha mapya!
 - b. Marafiki zetu wa zamani, wakati fulani hata familia zetu na majira ni zetu watatudhihaki jambo ambalo laweza kutufanya tuone aibu.
 - c. Tunapaswa kukumbuka kwamba Yesu alivumilia aibu ya kufa kwa ajili ya dhambi, pia.
 - d. Basi ikiwa tumefufuliwa toka kwenye kaburi la maji, tunatakiwa kuenenda mbele za uwepo wa Mungu kila siku.
 - e. Tunatakiwa kuwasiliana na Mungu kila siku kupitia maombi, kisha twaweza kukikaribia kiti chake cha enzi kwa ujasiri sasa hivi (Ebr. 4:16).
 - f. Tunatakiwa kumsikiliza Mungu kwa kupitia maneno yake katika Biblia, kwa kujifunza kila siku.

VI. Kila siku ya kwanza ya juma, chukua mkate usio tiwa chachu, na mzao wa mzabibu kwa kukumbuka kifo cha rafiki wetu (1 Kor. 11:24-25).

- A. Hatupaswi kusahau kamwe dhabihu yake kuu iliyofanya kwa heshima yetu.
 - 1. Mkate ni kwa ajili ya ukumbusho wa mwili wake ulioteswa.
 - 2. Mzao wa mzabibu ni kwa ajili ya ukumbusho wa damu yake iliyomwagwa.
- B. Tunatakiwa tuwe na shukrani kwamba Mungu hatuhitaji tufanya kama Yesu alivyofanya ili tuokolewe!
 - 1. Kile tu ambacho Mungu anahitaji kwetu ni kwamba tuzamishwe katika maji na tutoke majini ili kwamba tuweze kuishi maisha mapya yakijawa na matendo mema na upendo kwa Kristo na kwa wengine.
 - 2. Hatupaswi kufa kimwili kwa ajili ya dhambi, tunakufa kiakili kwenye dhambi.
 - a. Tunarekebisha akili zetu na kuzielekeza katika mema na mambo yaliyo sahihi, macho yetu yakimtaazama Yesu (Filip. 4:8-9).
 - b. Tunatengeneza njia yetu ya kwenda mbinguni tunapoezea nuru na wema kwa wote tunaonana nao njiani (Filip. 4:4-5).
 - c. Tunatakiwa kuishi kwa ajili ya Kristo tunapoishi hapa duniani na tukitazamia siku ambayo twaweza kuiacha dunia hii na kwenda kukaa milele na Yesu (Filip. 1:21).
- C. Yesu alikufa kimwili iliaweze kutuwasilisha kwa Mungu siku moja, kama watu watakatifu (waliolengwa toka kwenye dhambi) wasio laumiwa kwa maovu, na tuhuma zote (Kol. 1:21-23).
 - 1. Ni namna gani rafiki yetu alivyo tutendea jambo kuu!
 - 2. Kila asubuhu tuamkapo ni lazima tukumbuke kuinua msalaba wetu mabegani, kabla ya kutoka vitanda ni mwetu, na kutumia siku nzima kufa kwa ajili ya tuamaa za miili yetu na kwa ajili ya chukiza akili zetu.
 - 3. Tunatakiwa kumtaazama Yesu aliyetupatia njia ya kufanya hivyo, na kufuata mfano wake ambao kila mmoja wetu anaweza kufuata kwa kusoma katika Biblia.

VII. Tunatakiwa tukumbuke kwamba kama hatufi katika kutenda dhambi, basi tutakufa katika dhambi zetu (Yoh. 8:24).

- A. Tutakufa kwa namna moja au nyingine.

Mwana Kondoo Aliye Kimya

- I. Yohana Mbatizaji aliuambia ulimwengu kwamba Yesu alikuwa mwanakondoo (Yoh. 1:29)
- A. Alikuwa mwanakondoo ambaye angechukua dhambi za ulimwengu.
 - B. Mwanakondoo ni nini?
 1. Ni mtoto wa kondoo, kijana, siyo mkubwa anayeweza kuzaa watoto, ni mpole.
 2. Yesu asingekuwa na watoto au mke.
 3. Yesu alikuwa kijana na mpole.
 - C. Twaweza kusoma juu ya Yesu na kuona jinsi alivyokuwa mpole alipokuwa hapa duniani.
- II. Ni namna gani kondoo anaweza kuchukua dhambi ya ulimwengu?
- A. Yote yanaanza nyuma kwenye kitabu cha kutoka.
 1. Waisraeli walikuwa watumwa kwa Wamisri
 2. Walikuwa jirani na kuachiwa huru na ulikuwa usiku wao wa mwisho Misri
 3. Kifo kilitembea katika nchi nzima usiku ule.
 - a. Ilikukiepuka kile kifo walipaswa kuuu mwanakondoo na kuipaka damu ya mwanakondoo kwenye miimo ya milango ya nyumba zao.
 - b. Walipaswa waipike nyama ya mwanakondoo na kuila, wakijiandaa tayari kwa ajili ya safari.
 - c. Pasipo damu kupakwa kwenye nyumba yako, ungepata kifo nyumbani mwako.
 - d. Yeyote aliyekuwa mzaliwa wa kwanza, mtoto au mnyama angekufa, watoto au wakubwa (Kut. 12).
- III. Yesu ni mwanakondoo wetu wa pasaka, aliyetolewa dhabihu kwa ajili yetu (1 Kor. 11:6-8).
- A. Mwanakondoo wa Pasaka (Alipita Juu) ni nini?
 1. Mwanakondoo wa Pasaka ni jina ambalo Wayahudi walimwita mwanakondoo aliye chinjwa kwa ajili ya kukumbuka usiku ule mkuu walipoachiwa huru toka utumwani (Kut. 12:13)
 2. Malaika wa Mauti alipita juu ya nyumba zilizopakwa damu ya mwanakondoo kwenye milango, hivyo ndivyo alivyo mwanakondoo wa Pasaka (Alipita Juu).
 - B. Kuachiwa huru toka utumwani.
 1. Waisraeli waliachiwa huru toka utumwani, toka kwenye taifa ovu, na waliachiwa huru toka kwenye kifo cha mzaliwa wao wa kwanza.
 2. Yohana Mbatizaji alisema Yesu alikuwa mwanakondoo achukuaye dhambi ya ulimwengu.
 3. Paulo anasema katika (Rum 6:27, 18, 22, 23) kwamba dhambi ni mkuu wa utumwa.
 4. Wenye dhambi ni watumwa wa dhambi.
 5. Yesu alikuja kuwatoa watu toka kwenye utumwa wa dhambi.
 - C. Tukirudi kwenye 1 Kor., Paulo alisema kwamba Yesu alitolewa dhabihu kwa ajili yetu sawa na mwanakondoo. Ni namna gani mwanakondoo alivyo chinjwa?
 1. Mambo ya Walawi sura 1: Mwanakondoo aliletwa mbele ya makuhani
 2. Mwenye dhambi alipaswa kuweka mikono yake juu ya kichwa cha mwanakondoo, na kisha hukata kinywa cha mwanakondoo.
 1. Kuhani alichukua damu na kuimwaga madhabahuni, na kisha kumkata mwanakondoo vipande na kuviweka vipande madhabahuni na kuvichoma.
 - a. Huku ndiko kumwaga damu. Kumuuu mwanakondoo siyo vigumu, kwa sababu ni wapole sana.
 - D. Isaya 53:7, Isaya alisema kondoo alipaswa kuonewa na kuteswa, kwa kukamatwa na kuchinjwa kooni mwake. Anapoteza uhai wake bila ugomvi.
 1. Mdo. 8:22-24—Yule Mkushi alikuwa anajifunza mstari huu, bali hakuuelewa.
 2. Filipo akaja na kumfundisha juu ya Yesu, habari njema—kifo cha Yesu, mazishi na ufufuo wake.
 3. Kwa nini hii ni habari njema?
 - a. Kwa sababu alitolewa dhabihu ili kuiondoa dhambi yetu na kutuweka huru toka kifoni na dhambini.

- b. Sawa tu na Waisraeli Misri
 - c. Siku ya mwisho, Malaika wa Mauti atapita juu ya wale wote waliopaka damu ya mwanakondoo katika mioyo yao (Gal. 3:27).
 - E. Ilituweze kupaka damu ya Yesu kwenye mioyo yetu ni lazima tuzamishwe kwenye mioyo yetu, ni lazima tuzamishwe kwenye maji, ambamo ndimo tunagusana na damu yake
 - 1. Tunazamishwa kwenye damu ya mwanakondoo kimfano.
 - F. Kut. 12:22-23—Kama mtu yeyote alikuwa nje ya nyumba zao, alikuwa kwenye ulimwengu wa dhambi na mauti! Malaika wa Mauti angewapiga na kuwaua kama alikuwa mzaliwa wa kwanza.
 - 1. Rum. 6:1-3—panasema kwamba wote waliobatizwa ndani ya Kristo wamebatizwa katika mauti yake, hivyo tunawezaje kutenda dhambi na kuwa salama kutoka katika kifo cha milele?
 - 2. Ebr. 6:6—panasema kwamba yeyote anayeanguka kutoka kwenye usalama na kufanya dhambi (siyo kwa bahati mbaya) anamsulubisha mwanakondoo mara ya pili.
 - a. Wanamshikilia mwanakondoo ili aweze kudhihakiwa tena na waovu, sawa sawa na katika Mathayo 27.
- III. Kili siku ya kwanza ya juma, tunashiriki meza ya Bwana.
- A. Mkate usiotiwa chachu na mzao wa zabibu vinachukuliwa kwa ajili ya kukumbuka mwili na damu ya mwanakondoo.
 - B. tunafanya hivi kila siku ya kwanza ya juma badala ya kufanya mara moja kwa mwaka kwa sababu Mungu anasema hatujui ni lini atakapomtuma Yesu kwetu tena, ili atuchukuwe na kutupeleka kwenye nchi ya hadi yenye uhuru.
 - 1. Waisraeli waliambiwa wamle mwanakondoo wa pasaka, huku malizawa zote zikiwa zimewekwa tayari kwa ajili ya safari kwa sababu hawakujua ni lini ambapo Farao angewaambia watoke katika nchi yake.
 - C. Je, uko tayari kwa ajili ya ujio wa Yesu wa mara ya pili? Unaweza ukafa kabla hajaja mara ya pili, je, uko tayari kwa ajili ya kifo? Kama tukifa ni sawa tu kama vile Yesu akija, tutapumzika paradise paka Yesu atakaporudi.
 - D. Kama hatujajiandaa kama vile Wamisri, tutakufa milele.
 - 1. Yesu hatatuongoza kutupeleka kwenye nchi ya ahadi, mbinguni.
- IV. Ni lazima tukumbuke kwamba Yesu alijiruhusu mwenyewe kuwawa katika kifo chenye maumivu na kumwaga damu. Kwa nini?
- A. Ufu. 1:5—Ili atuokoa kutoka kwenye dhambi zetu kwa damu yake.
 - 1. Tunatakiwa tuwe watu wakulitukuza jina lake, kama vile wafanyavyo mbinguni (Ufu. 5:9).
 - a. Mwanakondoo anastahili!
 - 2. Ufu. 7:9-17—Kuoshwa katika damu ya mwanakondoo maana yake ni kwamba tutakuwa ndani ya nyumba ya Mungu, tukiwa pamoja na mwanakondoo, tutapokea baraka nyingi na maji ya uzima.
 - B. Kumtukuza mwanakondoo!
 - 1. Kumtukuza Yesu na dhabihu yake kuu!
 - 2. Kaa pale ambapo damu yake inakulinda.
 - 3. Usijaribu kwenda nje ya usalama wa damu yake ili utangetange kwenye ulimwengu na dhambi na mauti.
 - 4. Mogope sana Malaika wa Mauti.
 - 5. Usimchinje koo la Yesu kwa mara ya pili, usimsulubisha tena kwa mara ya pili!
 - C. Utazame juu ya msalaba kila siku na uone mwanakondoo aliyechinjwa na utubue dhambi na uendelee kubadilisha maisha yako ili umfurahishe Yesu.

Ufufuo

Mathayo. 28:1-20

- I. Kwa kuanza mwanzo wa maisha mapya, ni jambo zuri la kuritafakari.
 - A. Wote tunafanya makosa, na tunakusudia kuyaacha na tusingependa kuyarudia tena.
 - B. Pia kifo ni kitu ambacho tungependa tukibadilishe.
 - C. Kuna neno ambalo Biblia inalitumia mara nyingi: ufufuo.
 1. Maana yake ni kupulizia uhai mpya ndani ya mtu aliye kufa.
 2. Neno “ufufuo” ni neno zuri. Maana yake kuzaliwa mara ya pili. Lina leta tumaini na furaha kwenye roho.
- II. Kuna mifano kadhaa kwenye Biblia ya watu waliofufuliwa.
 - A. 1 Fal. 17:17-24—Nabii Eliya alimfufua mtoto wa kiume, toka kwa wafu.
 - B. 2 Fal. 4:32-37—Nabii Elisha alimfufua mtoto wa kiume mwingine aliye kuwa amekufa.
 - C. 2 Fal. 13:20-21—Maiti iligusa mifupa ya Elisha, na maiti ikafufuliwa toka kwa wafu.
 - D. Math. 8:5-13—Yesu alimfufua mtumishi wa akida.
 - E. Math. 9:23-26—Yesu alimrudishia uhai binti wa jumbe katika dunia hii.
 - F. Luka 7:12-16—Yesu alimfufua kijana toka kwa wafu.
 - G. Yoh. 11—Yesu alimfufua Lazaro kutoka kwa wafu.
 - H. Math. 27:52-53—Yesu alipokufa, wengi waliokufa na waliooza kwa muda mrefu walifufuliwa na waliishi tena.
- III. Yesu alizidi hatua moja zaidi ya kuwafufua wengine tu.
 - A. Siyo tu alikufa mwenyewe na kuzikwa, bali baada ya siku tatu, alijifufua kutoka kwa wafu. Hakika mwili wake ulikuwa tofauti.
 1. Aliweza kula samaki na rafiki zake, na bado aliweza kuonekana na kutoweka kwa wakati uo huo.
 2. Kwa wakati huo alikuwa kati ya mbinguni na duniani.
 - B. Tufufuliwapo kutoka kwenye kaburi la maji ya ubatizo tunafanana naye kulingana na Rum. 6.
 1. Tunatakiwa tuwe tofauti hakika.
 2. Twaweza kula na kuishi hapa, bali tunataki wa tutoweke katika dhambi na tuonekane katika haki.
 - a. Tunaweza kutoweka wakati uo huo dhambi igongapo mlangoni petu.
 - b. Twaweza kwonekana wakati uo huo matendo mema yajapo na kugonga kwenye mlango wetu.
 3. Pia, tunasubiri, kwa ajili ya muda upasao tutakapo paa mbinguni kama vile Yesu, na hakika kuwa kiroho mbele za uwepo wa Mungu.
 - C. Yesu alifufuliwa kutoka kwa wafu, na anatuamru na sisi tufufuliwe kutoka kwa wafu, pia.
 1. Tunatakiwa tufufuliwe kwenye upya wa uzima. Tunatakiwa tuanze upya.
 2. Sisi wakristo tunafufuliwa tunapo panda kutoka kwenye maji ya ubatizo.
 - a. Maisha mapya yana maanisha kwamba tunaanza upya.
 - b. Maana yake ni kwamba tunabadilika kwa yale tuliyokuwa tunayafanya, badala yake tunaanza kufanya mengine.
 - c. Unapoanza upya, ni lazima uenende tofauti.
 3. Ni lazima watu wajue kwamba uko tofauti.
 - a. Kama hawaoni badiliko lolote, hapo hujaanza upya.
 - b. Baada ya ubatizo, kama unaendelea kufanya mambo yale yale uliyokuwa unayafanya na kwa namna ile ile, hapo hujafufuliwa.
 - c. Hapo umezamishwa tu kwenye maji na umeoga tu.
- IV. Ni nini tunachopaswa kufanya baada ya ubatizo kilicho tofauti? Kwanza kabisa tuangalie kile tulicho kuwa tunakifanya.
 - A. Kabla hatujawa wakristo tulikuwa tunafanya mambo ya ubinafsi (Gal. 5:19-21).
 - B. Mungu anatuambia sasa kwamba tunapaswa kuacha kufanya mambo hayo na kuanza kufanya mambo ambayo siyo ya ubinafsi (Rum. 12:9-21).
 - C. Tunatakiwa kuutamia muda tunaoweza kwenda mbinguni. Tunatakiwa kutazamia wakati ambao Yesu atarudi tena (Tit. 2:13; 2 Pet. 3:12).

- D. Tunatakiwa tuwe watu wa kutafuta njia za kuwatia moyo watu ili wawe imara katika Bwana (Ebr. 10:23-25).
- E. Tunatakiwa tuwe watu wa kujaribu kumsihi Mungu kwa sababu yeye ndiye aliyetufufua.
- V. Tunaweza kumtazama Yesu kama mfano wetu juu ya kile tunachotakiwa kukifanya katika maisha.
- A. Yesu alikutua muda wake wote kufikiri juu ya wengine.
1. Alipokuwa mtoto, alikuwa mtiifu kwa wazazi wake watauwa, na aliwaheshimu wengine.
 2. Katika huduma yake aliwafundisha wengine, aliwaponya wengine, aliwafufua watu kutoka kwa wafu, aliwasamehe wengine, aliwahubiria wengine neno la Mungu, alitumia muda mwingi kumwomba Mungu.
 3. Alikufa kwa ajili ya wengine.
 4. Sasa yuko mbinguni akiwa mwanasheria wetu, akitulinda dhidi ya tuhuma za Shetani, bado anafikiri juu ya wengine.
- B. Kwa hiyo kwa kuwa yeye ni mfano wetu, tunatakiwa tufanye vivyo hivyo.
1. Tunatakiwa kuwafundisha wengine, na tunatakiwa kuwasaidia wengine wanapokuwa na wakati mgumu, tunatakiwa kuwahubiri watu juu ya mapenzi ya Mungu, na tunatakiwa kuwalinda watu dhidi ya Shetani.
 2. Tunatakiwa tuwapende watu kama vile Yesu alivyowapenda watu.
 3. Tunatakiwa tuwe tayari kufa kwa ajili ya Yesu kama vile alivyo kuwa tayari kufa kwa ajili yetu.
- VI. Je, umewahi kufikiri juu ya watu wale wote ambao Yesu aliwaponya alipokuwa hapa duniani?
- A. Kama binti wa yule jumbe (Math. 9:23-26). Alipofufuliwa, kila mtu alimwambia habari ya kusema nini kimetokea, na ni nani aliye mrejesho toka kifoni?
1. Ni jinsi gani alivyo kuwa? Je, alichukua nafasi yake ya pili ya uhai na kuwa mtu mwema?
- B. Kisha kulikuwa na mtumwa wa akida, ambaye Yesu alimfufua kutoka kwa wafu. Alikuwa je kabla hajafa?
1. Alifanya nini na nafasi yake ya pili?
- C. Rum. 12:1-2—Mungu anampatia kila mmoja wetu nafasi ya pili kila siku!
1. Zitakuwepo nyakati ambazo tutasahau kwamba tunaishi maisha mapya, na tutafanya mambo ambayo tulikuwa tunayafanya zamani (Rum. 1:28-32).
 - a. Tuwapo kwenye dhambi tunastahili mauti, tunakuwa wafu kwa Mungu (Efe. 2:1-6).
 2. Lakini ikiwa tu, tunauzima katika miili yetu. Mungu anatupatia muda na nafasi ya kufikiri tena juu ya maisha yetu na kuanza upya tena.
 - a. Kwa kuwa dhambi inazaa mauti, kila siku tuna nafasi ya kufufuka upya wa uzima.
 3. Je, hiyo siyo zawadi ya ajabu kutoka kwa Mungu?
- D. Lakini, watu wengi wanajisikia kwamba wakati wote wanao ulimwenguni ili kubadilisha maisha yao.
1. Yak. 1:3-17—Tunapofikiri kwamba wakati wote tunao ulimwenguni, tunakuwa tumepotea sana.
 2. 2 Kor. 6:2—wakati wa wokovu ni sasa wala siyo kesho.
 3. Filip. 2:12—Paulo anasema wokovu unatakiwa kutimizwa kwa hofu na kutetemeka!
 - a. Siyo mchezo wa kucheza, ni uzima au kifo.
- VII. 1 Pet. 1:22-25—“Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo, KWA KUWA MMEZALIWA MARA YA PILI, SI KWA MBEGU IHARIBIKAYO, BALI KWA ILE ISIOHARIBIKA...mwili wote ni kama majani...”
- A. Ufufuliwe toka kwa wafu kupitia ubatizo. Endelea kukaa katika hali ya ufufuo kupitia utii. Endelea kutazama mbinguni. Kaa katika hali ya wokovu.

Kanisa: Mwili Wa Yesu

Mat. 24:30; Yoh. 14:1-3; Matendo 1:9-11; 1 The. 4:13-18; Ufu. 1:7-8

I. Katika semina hii, tumeangalia sura nzima ya kifo cha Yesu.

A. Sasa twaweza kuuona mwili wake kwa dhahiri kabisa. Twaweza kuona:

1. Mwili wake ukisalitiwa na rafiki, na ukitiliwa mashaka na Viongozi wa Kidini, watu waliopaswa kuwa wafanyakazi wa Mungu.
2. Mwili wake ukivumilia mateso kutoka kwenye maneno, dhihaka, ngumi, mikono, mijeredi, miiba, na hata kuchukua msalaba mpaka mlimani nje ya mji.
3. Mwili wake ukigongomewa mtini uliokuwa kwa namna ya msalaba.
4. Mwili wake ukipoteza uhai.
5. Mwili wake unazikwa kwenye kaburi la tajiri.
6. Mwili wake unafufuliwa na kutembea kati ya watu, kufundisha, ukila na kushauri.

B. Hakika mwili huo tunaoweza kuuona ni sisi. Sisi ndio mwili huo (Efe. 5:30; Kol. 1:18)

II. Mdo. 9:1-6—Mtu aliyelitwa Sauli aliwahiribu watu waliomfuata Yesu.

A. Yesu alimsimamisha njiani na kumwambia kwamba yeye (Sauli) alikuwa anamuudhi Yesu!

1. Sauli, kwa kuwatesa na kuwauwa watu ambao Mungu alikuwa amewaongeza kanisani mwake, hakika alikuwa akimtesa na kumuua Yesu!

B. Maana yake nini kuwa mshiriki wa mwili wa Yesu? (Kol. 3:1-4) Kila siku:

1. Tunatazamia juu ya ukweli ule wa kwamba sisi ni viungo wa mwili wa Kristo.
2. Tunafikiri sana juu ya kuenenda katika njia iendayo kwenye mlima wa kifo, tukibeba misalaba yetu pembeni mwa Yesu.
3. Tunagongomewa kwenye mti wa tamaa za maovu yetu, na mawazo yetu maovu.
4. Tunazika asili zetu za maovu na tukitazamia katika kujifufua katika upya wa uzima.

C. Efe. 1:22-23—Yesu ndiye kichwa cha mwili.

1. Kila kiungo ni lazima kifanye kazi zaidi, kuliko tu kupokea kutoka kwenye viungo vingine.
2. Hakuna kiungo hata kimoja, cha binadamu au cha mwili wa mnyama ambacho kinachukua tu na kamwe hakitoi.
3. Kiungo cha mwili kinapopokea tu, na kamwe hakitoi, kiungo hicho hakifai.
 - a. Kiungo hicho hakifanyi kazi yake ili kufanya mwili ufanye kazi yake vizuri.
 - b. Kiungo hicho hakijakiangalia kichwa cha mwili.

D. Kwa nini tuatakiwa kukiangalia kichwa cha mwili?

1. Kichwa kina ubongo.
 - a. Ndicho kiini cha wazo linalo usaidia mwili ufanye kazi kiufasaha.
 - b. Ubongo unaratibisha ujumbe wote kutoka kwenye viungo na mazingira.
 - c. Ubongo unaweza kuviambia viungo vyote vya mwili cha kufanya.
2. Kiungo cha mwili kinapokuwa hakiangalii kwenye kile ambacho kichwa kinamru, hapo kiungo hicho cha mwili kinakuwa kimekufa.
 - a. Kiungo hicho cha mwili kinakuwa kimejitenga chenyewe toka kwenye mwili.
 - b. Kinatakiwa kiondolewe au kinakuwa hatari kwa mwili, kwa sababu kitu ambacho kimekufa kitaoza na kitasababisha maumivu, madhara, homa, hatimaye kifo.

E. Wote tumejisikia maumivu kwenye miili yetu, siyo?

1. Jino linapoanza kuoza linasababisha maumivu makali mdomoni na linaweza kusababisha maumivu ya masikio, na maumivu ya kichwa, na kukosa usingizi usiku. Linatakiwa kutibiwa, au kung'olewa vinginevyo litasababisha madhara.

III. Efe. 1:22-23—Mungu alimpa Yesu kazi ya kuwa kichwa cha kanisa, mwili wake.

A. Kuliambia kanisa juu ya kile ambacho linaweza kufanya au ambacho haliwezi kufanya, siyo kazi ya mwanaume au mwanamke.

1. Kiungo cha kanisa, kinapoanza kujiinua na kujifanya ndicho kichwa cha viungo. Na kuanza kuweka amri na sheria ambazo hazipo kwenye maandiko, kiungo hicho kimekufa.
 - a. Viungo vingine vinatakiwa kufanya chochote juu ya kiungo hicho, wakati uo huo, vinginevyo mwili utapata “homa” na kuwanza kuhangaika maishani mwake.
 2. Kama mshiriki wa kusanyiko anajisikia kwamba ni tajiri, kila mtu ni bora amwambie mtu huyo kwamba amekufa.
 - a. Kama washiriki wa kusanyiko hilo hawaelewi kwamba, kiungo kikifa wanatakiwa kushughulika nacho, hapo kusanyiko hilo laweza kuteseka.
 3. Kila mtu aliye nje ya kanisa analiangalia kanisa, na wanaliona kama kichekesho!
- B. Wote tunaelewa jinsi inavyokuwa kama moja ya viungo vyetu vya mwili vikifa.
1. Jambo hilo linapotokea tunakwenda hospitalini, tunamtafuta mganga ili tutibiwe.
 2. Marko 2:17—Yesu ndiye mganga mkuu.
 - a. Yeye ni mganga wa wagonjwa, wenyedhambi.
 - b. Dhambi ni mauti (Rum. 6:23), kwa hiyo wakristo wanaofanya dhambi ni wagonjwa wanaumwa sana.
 - c. Yesu atafanya kinachoweza kufanya mwili wake uwe na afya.
- C. Viungo vinavyoacha kufanya kazi zao katika mwili, katika kanisa, vina visababu vingi sana.
1. Hata hivyo, sababu yao kuu ni kwamba kwa sababu wameacha kufanya kazi kwa ajili ya Yesu na wameanza kujiangalia wenyewe na tamaa zao.
 - a. Watu wengine wanatamani kulala ndani na wala siyo kwenda ibadani kwa Kristo.
 - b. Watu wengine wanatamani kutengeneza pesa ambazo ni muhimu sana kwao, kuliko kumwabudu Kristo na kufanya kazi na washirika wengine.
 - i. Hakuna kosa lolote kwa kutengeneza pesa, lakini kwa kufanya kazi kutengeneza pesa na kuliacha kanisa na kumpuuza Yesu ni dhambi.
 - c. Kuna watu wengine, wanatamani kucheza. Pengine ni katika michezo au baa, au kuwatazama watu wengine wanapocheza, na wanashinda ibadani au wanashinda kufanya kazi na washiriki wengine wa mwili kwa kufanya kazi ya Bwana.
 - d. Watu wengi wanatamani kufanya kazi za mashambani kwao kuliko kufanya kazi katika mwili wa Kristo.
 - i. Ardhi ni muhimu zaidi kwao kuliko aliyeifanya ardhi.
 - ii. Kusingekuwa na tatizo lolote kusimama kufanya kazi kwa masaa kadhaa kwa jumapili asubuhi na kwa lisaa lichoja kwa mchana kwa kulitembelea kusanyiko lingine na kumwabudu Mungu na viungo vya mwili.
 - iii. Mungu atawabariki kwa kuwa wafanyakazi wazuri wa mwili wake.

IV. 1 Kor. 12:27—Kanisa ni mwili wa Kristo, na sisi ni viungo vyake kila mmoja.

- A. Tunatakiwa tufanye kazi pamoja ili tuwe na umoja wote kwa kufanya mapenzi ya Mungu.
- B. Tunatakiwa tufanye kazi kwa pamoja na kuzifisha dhambi katika maisha yetu msalabani.
- C. Tunatakiwa tufanye kazi kwa pamoja kwa kuyazika maovu, na kujifufua kila siku kwa kutenda mema.
- D. Matendo haya ni lazima yaendelee katika mwili wa Kristo kila sekunde. Viungo vyote kila wakati vifanye kazi kwa pamoja ili viufanye mwili uwe hai na wenye afya. Viungo vinasaidiana! Vinafanya kazi pamoja kwa lengo moja: tubakie hai kwa Kristo kwa kubakia wafu kwenye dhambi. (Ebr. 10:22-27; 2 Pet. 1:5-11).

Marejeo Ya Pili

- I. Moja ya sehemu ya injili ni kurudi kwa Kristo mara ya pili. Anarudi tena.
- A. Baada ya ufufuo wake, Yesu alipaa hewani ili aende kukaa katika mkono wa kuume wa Yehova Mungu (Mdo. 1:9-11).
 - B. Malaika waliwaambia wafuasi wake kwamba, Yesu atarudi tena namna ile ile aliyo paa.
 - 1. Hii inamaanisha kwamba kutakuwa mawingu.
 - 2. Yesu ataonekana siku moja na macho yote yatainuliwa kumwona, kutoka ulilmwenguni kote watamwona mawinguni (Yoh. 1:32-33).
 - C. Yesu aliwaambia watu kwamba watavutwa naye atakapoinuliwa, na Yohana anasema Yesu alikuwa anaongelea kifo chake msalabani.
 - 1. Misalaba iliwainua waharifu juu sana ili kwamba watu wote wawatazame na wawaone hata wakiwa kwa mbali.
 - 2. Ili tuweze kuokolewa ni lazima tuutazame msalaba na kumwamini Yesu na kumtii kwa kubatizwa ndani ya maji (Yoh. 3:3-5; Math. 28:19-20).
 - 3. Katika ukamilifu wa dahari, Yesu ajapo tena hatainuliwa tena msalabani, bali atakuwa juu mawinguni na macho yote yatainuliwa kumwona kule (Ufu. 1:7).
 - 4. Ajapo tutavutwa kwake kwa sababu atakuja kuwachukua watu wake na kuwapeleka nyumbani kwao kwa milele.
 - 5. Wale wote ambao hawaja chukua nafasi zao nyingi ili wafanyike kuwa watu wake watakimbia na kujificha na kutamani miamba iwafunike (Ufu. 6:15-16).
- II. Ahadi za Yesu
- A. Yesu alitunza ahadi zake nyingi sana, na alitunza unabii 364 wa Mungu unaohusu kifo chake.
 - 1. Twaweza kuhakikishiwa kwamba Yesu atatunza ahadi yake ya kurudi tena.
 - B. Math. 24:30-31—
 - 1. Anasema atakuja katika mawingu, na nguvu na utukufu mkuu.
 - 2. Atawatuma malaika zake na tarumbeta kuu ya wito, kama vile jemadari atumavyo makundi yake (1 Thes. 4:16-18).
 - 3. Malaika watakusanya watu wote waliotii amri za Yesu.
 - C. Math. 24:36—Yesu anasema kwamba kuhusu siku ile na saa, hakuna ajuaye, hata malaika, hata Yesu mwenyewe hajui. Yehova Mungu tu ndiye ajuaye, kama vile siku za Nuhu.
 - D. Math. 24:39—Watu wengi watajisahau.
 - 1. Lakini wakristo wanatakiwa kuwa waangalifu sana kwamba Yesu anaweza kurudi wakati wowote (Tit. 2:11-14; 1 Thes. 5:4).
 - 2. Tunatakiwa kuishi maisha yetu katika hali ya kujua kwamba Yesu anaweza kurudi wakati wowote na kwamba tunaweza kuinua macho yetu kwa furaha na kuweza kuonana naye kwa kumlaki (2 Pet. 3:11-14).
 - 3. Tunatakiwa kuitazamia siku ile kwa shauku, tukiifurahia, na tukiwa tayari kwa ajili ya hiyo (Ufu. 22:20).
 - 4. Efe. 5:15-17—Tunatakiwa kuukomboa wakati wetu maana zamani hizi ni za uovu.
 - E. Filip. 1:21—Kuishi kunatakiwa kuwe kwa ajili ya Kristo na kufa kuwe faida.
 - 1. Je, twaweza kusema hivyo juu yetu wenyewe?
 - F. Ebr. 11:16—Tunatakiwa tuwe tunatazamia kuishi katika nchi ya Mbinguni, na tujisikiapo hivyo Mungu haoni aibu kutuita watu wake!
- III. Kanisa la mji wa Thesalonike liliutazamia ujio wa Kristo.
- A. Bali wautazamia kwa shauku sana hata hawaona siku walizokuwa wanaishi ndani yake.
 - 1. Waliamini kwamba Yesu atarudi haraka sana. Lakini awakuelewa kwamba Yesu hafungwi na muda na “haraka” inaweza kumaanisha miaka mingi (2 Pet. 3:8).
 - 2. Waliuza nyumba zao, waliacha kazi zao, na walikaa tu wakimsubiri Yesu.
 - 3. Pengine walikuwa wanatazama mbinguni wakimngojea.
 - B. Kusudi lao lilikuwa zuri, lakini matendo yao hayakuwa mazuri.
 - 1. Yesu mwenyewe alisema hakuna mtu ambaye angejua ni lini atarudi.
 - 2. Alisema kwamba arudipo wote tutakuwa tunafunaya kazi na shughuli za kila siku.
 - 3. Alisema kurudi kwake kutakuwa kwa kushangaza kabisa.

- a. Kuwa tayari kwa ajili ya ujio wa Yesu hakumaanishi kwamba tukae tu bila kazi yoyote na kutumai kwamba leo ndiyo siku yenyewe (2 Thes.2:16-17; 2 Thes. 3:13; 1 Kor. 15:58)
 - b. Yesu alisema tufanye kazi madamu ni mchana (Efe. 5:15-16; Yoh. 9:4).
 - C. Filip. 1:21—Kuishi duniani kunatakiwa kuwe kwa ajili ya Kristo na kufa kunatakiwa kuwe bora kuliko kitu cho chote duniani.
 1. Paulo alipokuwa hai alifanya kazi ya kueneza injili ya Kristo kwa bidii sana.
 2. 1 Thes. 2:12; Efe. 4:1—Kuishi kwa ajili ya Kristo tuwapo hapa duniani ndio wito tulio itiwa.
 3. Kol. 1:10—Paulo anasema tunatakiwa tuenenda kama ulivyo wajibu wetu kwa Bwana.
 4. Tunatakiwa tuwe tunampendeza Bwana hakika.
 5. Tunatakiwa tuwe tunapata matokeo katika kila tendo jema tunaloweza kulifanya.
 6. Tunatakiwa tuwe tunakuwa katika kumjua Mungu (2 Pet. 1:5-11).
- IV. Yesu anatuambia habari nyingi sana juu ya kurudi kwake mara ya pili.
- A. Math. 25:1-13—Wanawali kumi
 1. Watano kati ya wale wanawali walikuwa wamejiandaa kikamilifu walikuwa tayari kwa ajili ya arusi.
 - a. Walikuwa wamefikiri juu ya uwezekano wa kusubiri kwa muda mrefu.
 - b. Mara nyingi sherehe za arusi zinachukua muda mrefu kuliko zilivyo kusudiwa.
 2. Wanawali wengine watano walikuwa wamejiandaa kusubiri kwa muda mfupi tu.
 - a. Wanawali ambao hawakujiandaa waliishiwa “mafuta” ili waendeleo kuziwasha “taa” zao.
 3. Yesu alisema SISI ni nuru (Math. 5:14-16).
 - a. Tunatakiwa tutunze “nguvu” zetu ili kwamba tutunze “taa” zetu ziendeleo kuwaka kwa mwanga mkuu, mpaka Yesu ajapo ambaye ndiye bwana arusi atakapokuja kutuchukua na kutupeleka katika jumba lake la kifalme hatupaswi tuchoke katika kutenda mema (Gal. 6:9-10),
 - B. Math. 25:14-30—Bwana mmoja na wafanyakazi wake watatu.
 1. Bwana huyu anawaambia wafanyakazi wake watatu wafanye kazi yeye akiwa ameondoka.
 2. Huyu bwana hakujua ni lini atarudi, lakini alitegemea kwamba watu wake wafanye kazi.
 - a. Wawili kati ya watu wale walitii na walipata matokeo mazuri kutoka kwenye kazi yao.
 - b. Yule mtu wa tatu aliacha kufanya kazi.
 3. Bwana aliporudi, alimfukuza mwajiliwa wake watatu na kumwita mtu mvivu.
 - a. Yesu anatuambia tufanye kila tuwe zacho katika jina lake pindi tuwapo hai.
 - b. Hapo tu, na ndipo tutakapokuwa na furaha tukimwona Yesu anarudi.
- V. Tunapaswa kumsubiri Mwana wa Mungu kutoka mbinguni.
- A. Yesu atatuokoa na ghadhabu ijayo siku ya mwisho (1 Thes. 1:10).
 - B. Tunaposubiri, tunatakiwa kufanya kazi za Mungu na hatutakiwi kuichoka.
 - C. 1 Thes. 3:12-13—Paulo aliomba baraka juu ya kanisa la Thessalonike.
 1. Alimwomba Mungu awasaidie wakristo na waongezeke katika kuonyesha upendo wao kwa wao na kwa watu wote.
 2. Ukifa kabla hajarudi, unatakiwa uwe mmoja wa wale makutano makuu ya roho za watu watakao fufuliwa na Yesu kwanza toka ardhini!
 3. Kama utakuwa hai, utakuwa mmoja wa wale makutano makuu ya watu ambao Yesu atawanyakua na kumlaki mawinguni!
 - a. Tena ni mwonekano wa ajabu kiasi gani huo utakuwa!
 - b. Mwonekano huo wa ajabu, siku hiyo ya ajabu, ndiyo sababu ya kifo, mazishi, na ufufuo wa Yesu Kristo. Hiyo ndiyo sababu kuu ya mateso yake ambayo tumejifunza. Tafadhali, muishi maisha yenu ili muweze kuwa pamoja na roho zitakazo mlaki Yesu mwawinguni kwa furaha kuu!

